**St.Vincenti shule ya watoto viziwi,iliyopewa cheti cha ubora wa elimu**

**Na Albano Midelo**

St.Vinsenti Shule ya Msingi ya elimu maalum ya wenye ulemavu wa kusikia iliyowahi kupewa cheti cha ubora wa shule Tanzania mwaka 2000 kutoka Wizara ya Elimu kutokana na kufaulisha karibu kila mwaka darasa zima.



Shule ya mtakatifu Vincenti inayomilikiwa na watawa wa kanisa katoliki imeanzishwa katika Kata ya Ruhuwiko Manispaa ya Songea Mkoa wa Ruvuma.

Shule hiyo imejengwa katika viwanja ambavyo vilitumiwa na aliyekuwa Kiongozi Mkuu wa Kanisa Katoliki Duniani Hayati Papa Yohanne PauloII, mwaka 1990 katika adhimisho la misa takatifu.Hayati papa yohanne Septemba 1990 alifanya ziara ya kutembelea nchi kadhaa barani Afrika ikiwemo Tanzania.

Miongoni mwa mikoa ambayo kiongozi huyo wa ngazi ya juu wa kanisa katoliki Duniani aliweza kuitembelea na kufanya adhimisho la misa takatifu ni eneo la Ruhuwiko mjini Songea Mkoa wa Ruvuma.

Kutokana na umuhimu wa ujio wa papa Yohanne Paulo Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Songea liliona umuhimu wa eneo hilo kuweka kumbukumbu ya ujio wa Papa ndiyo maana

ikapendekezwa kujengwa shule ya bweni ya wenye ulemavu wa kusikia yaani viziwi inayoitwa St.Vincenti.

Mkuu wa Shule hiyo Sr.Anna Mgaya anasema St.Vincent ni miongoni mwa shule ambazo zinatoa mchango mkubwa kwa wenye ulemavu hapa nchini inahudumia watoto wenye ulemavu katika kundi la viziwi.

Anabainisha kuwa shule hiyo inawahudumia watoto wenye ulemavu viziwi kutoka mikoa mbalimbali nchini ikiwemo Ruvuma, Njombe, Iringa, Mbeya,Dar es salaam,Rukwa na Mtwara.

Kwa mujibu wa Sr.Mgaya shule ya St.Vinsenti ilianzishwa mwaka 1984 na Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Songea baada ya kufanyika makubaliano kati ya kanisa na serikali.

“Makubaliano hayo yalifanyika baada ya kufanyika utafiti na kugundulika kuwa wapo watoto wengi viziwi katika ukanda ya kusini ambao wanakosa nafasi ya shule baada ya ukanda mzima wa kusini kutokuwepo kwa shule ya wenye ulemavu viziwi”,anasema.

Shule hiyo ilipata usajili Januari 15,1989 na kupewa namba RV/01/02/033 na ilifunguliwa rasmi na Waziri Mkuu Mstaafu hayati Rashid Mfaume Kawawa Februari 2,1992 ambaye siku ya ufunguzi alipanda mti wa kumbukumbu ambao bado upo hadi leo.



Kulingana na Sr.Mgaya shule hiyo ina uwezo wa kupokea wanafunzi wasiozidi 200 tu na kwamba kutokana na hali hiyo Kila mwaka watoto wanye ulemavu viziwi wengi wanakosa

nafasi ya kujiunga katika shule hiyo kutokana na shule kukosa uwezo wa kuchukua wanafunzi wengi zaidi ya hao.

“kutokana na changamoto zilizopo idadi ya wanafunzi waliopo hivi sasa katika shule yetu ni 140 ambao wanasoma kuanzia shule ya awali hadi darasa la saba”anasema na kuongeza kuwa shule hiyo ina kitengo cha ufundi katika fani za useremala,ushonaji,upimaji na utengenezaji wa shime sikio kwa ajili ya kuongeza usikivu kwa viziwi.

Ameyataja baadhi ya mafanikio yaliopatikana tangu kuanzishwa kwa shule hiyo kuwa ni shule kujitosheleza katika majengo na samani,vifaa vya kujifunzia na kufundishia mazingira mazuri ya kujifunzia,kufundishia na nyumba za walimu zinazokidhi mahitaji ya walimu.

Sr.Mgaya anasema shule hiyo inafanya vizuri kitaaluma ambapo kila mwaka karibu wanafunzi wote wanachaguliwa kuendelea na masomo ya sekondari katika shule zinazochukua wanafunzi wenye ulemavu zikiwemo za Njombe na Iringa.

“Kwa mfano matokeo ya mwaka jana ya darasa la saba yanaonesha kuwa wanafunzi waliofanya mtihani walikuwa 19,wanafunzi wote walifaulu, shule yetu ngazi ya wilaya ilishika nafasi ya saba kati ya shule 75,kimkoa ilikamata nafasi ya 78 kati ya shule 729 na kitaifa shule ilikuwa ya 1854 kati ya shule 15,867”,anasema.



Shule hiyo ina kitengo cha ufundi ambacho kinatoa mafunzo ya awali katika fani za useremala na ushonaji na kufanya mitihani ya VETA na kupewa vyeti vya ufundi kila mwaka.

Shule hiyo pia imeanzisha darasa la kompyuta ili kuendana na Ulimwengu wa Sayansi na teknolojia kutokana na ukweli kuwa wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia wana uwezo mkubwa katika masomo ya vitendo hivyo wanaweza kufanya vizuri katika somo hilo.

Utafiti umebaini kuwa shule kwa ajili ya watu wenye ulemavu hapa nchini bado ni changamoto kubwa kutokana na ukweli kuwa hadi sasa kuna shule chache huku nyingi zinamilikiwa na taasisi binafsi na mashirika ya dini licha ya kwamba idadi ya watu wenye ulemavu inaendelea kuongezeka.

Kwa mfano Halmashauri ya manispaa ya Songea ina shule 10 zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum kati ya hizo shule moja tu ni ya sekondari ambayo ni shule ya sekondari ya wavulana Songea.

Manispaa ya Songea ina vitengo nane katika shule za msingi za serikali na shule moja maalum ya bweni ya mtakatifu Vincenti inayomilikiwa na kanisa katoliki.

Afisa elimu Maalum wa Manispaa ya Songea Rehema Nyagawa amezitaja shule za msingi zenye vitengo vya elimu maalum kuwa ni Luhira, Chandarua, Mitawa, Mahiro, Ndilimalitembo, Subira,Mfaranyaki na Chemchem.

kulingana na takwimu za Idara ya Elimu ya Manispaa hiyo hadi kufikia Mei,2016 katika shule hizo kuna jumla ya wanafunzi 328 wenye ulemavu wa aina mbalimbali ukiwemo viziwi, ngozi, akili,viungo na wanafunzi wenye ulemavu zaidi ya mmoja.

Takwimu za wenye ulemavu katika Mkoa wa Ruvuma kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 inaonesha kuwa kuna watu 523 wenye ualbino,wasioona zaidi ya 20,000,viziwi zaidi ya 12,000,wenye ulemavu wa viungo zaidi ya 15,000,,wenye ulemavu wa akiri 14,000 na wenye aina nyingine za ulemavu karibu 5000.

Tanzania imekuwa na ongezeko kubwa la watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali ambao wanahitaji mahitaji maalum ya elimu,miundombinu na mahitaji mengine.

Kulingana na sensa hiyo Tanzania ina zaidi ya watu 16,000 wenye ualbino,wasioona zaidi ya 848,000,viziwi zaidi ya 425,000,ulemavu wa viungo zaidi ya 525,000,ulemavu wa akiri zaidi ya 400,000, na karibu 100,000 wana ulemavu wa aina nyingine.

**Albano Midelo ni mwanahabari anayechangia katika gazeti hili anapatikana kwa baruapepe albano.midelo@gmail.com, simu 0784765917**